

Mipango kadhaa ya sera toka mwanzo hadi mwisho, iko katika hali ya maendeleo] Kwa mfano, Kituo cha Teknolojia ya hali ya angana mtandao inanzishwa chini ya UNFCCC. Sambamba na hili, wafadhili kama vile Idara ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa wameanzisha vituo vya uvumbuzi katika nchi zinazoendelea. Hizi hutoa uwezekano wa kubaki kabisa juu-chini au kujihusisha katika njia zenye utaratibu zaidi ambazo zinatafuta kuelewa na kukabiliana na mahitaji ya ndani na matukio. Kwa sasa, matokeo yote mawili lazima yatafanyika.

“Mtazamo wetu ni ... kutoa uchambuzi ambao unaweza kusaidia kuunda maendeleo ya njia za usawa zaidi na endelevu za nishati katika siku zijazo”

Mtazamo wetu katika STEPS Centre ya Nishati na Kiocha cha Mabadiliko ya hali ya anga ni kuelewa jinsi njia za nishati katika nchi zinazoendelea, hasa zile ambazo zingeweza kufaidi nchi maskini na hasa zile zisizojiweza zimejitokeza kihistoria ili kutoa uchambuzi ambao unaweza kusaidia kuunda maendeleo ya usawa zaidi na njia endelevu za nishati katika siku zijazo.

Kusoma zaidi

Energy Pathways in Low-Carbon Development: From Technology Transfer to Socio-Technical Transformation, STEPS Working Paper 46, imeandikwa na Rob Byrne, Adrian Smith, Jim Watson na Daudi Ockwell (2011). ISBN 978-1-78118-000-6

“Dynamic Sustainabilities: Technology, Environment, Social Justice” imeandikwa na Melissa Leach, Ian Scoones na Andy Stirling, 2010, Vitabu vya Earthscan. ISBN 9781849710930

Vitabu vingine, magazeti na maswala ya mjadala na maelezo katika mfululizo huu zinapatikana katika www.steps-centre.org

Utambuzi

Maelezo haya yaliandikwa na Rob Byrne na kuhaririwa na Julia Day.

Kuhusu STEPS Centre

STEPS Centre (Jamii, Teknolojia na Njia za Mazingira kwa Uendelevu) ni utafiti interdisciplinari wa kimataifa na kitovu cha shughuli za sera inayounganisha masomo ya maendeleo na masomo ya sayansi na teknolojia. Tunalenga kuendeleza mbinu mpya ya uelewa, hatua na mawasiliano kuhusu uendelevu na maendeleo katika zama za mabadiliko makubwa ya nguvu. STEPS Centre iko katika Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo na Sera ya Utafiti wa SPRU wa Sayansi na Teknolojia katika Chuo Kikuu cha Sussex na mtandao wa washirika katika bara la Asia, Afrika na Marekani ya Kusini na inafadhiliwa na Baraza la Uchumi na Utafiti wa Jamii. Kujua zaidi: www.steps-centre.org

Wasiliana Nasi

STEPS Centre,
Institute of Development Studies,
University of Sussex, Brighton
BN1 9RE, UK
+44 (0)1273 915673
Barua pepe: steps-centre@ids.ac.uk
Tovuti: www.steps-centre.org
Twitter: @stepscentre



Njia za Nishati katika Ustawi wenye Kaboni-Kidogo

Kutoka kwa Karatasi ya mjadili 46 ya STEPS:

Njia za Nishati katika Maendeleo yenye Kaboni-Kidogo:

Kutoka Uhamisho wa Teknolojia hadi kwa Mabadiliko ya Kiufundi-ya Ujamaa

Nishati na maendeleo zinaendanisha pamoja: taa, kupika, uhamaji, kupasha joto, kupoza na mawasiliano zote ni muhimu kwa michakato ya maendeleo. Aidha, kwa namna ambayo huduma za nishati zinavyotambuliwa zina madhara mazuri na na mabaya kwa afya zetu, mazingira, mali na mahusiano ya ujamaa.

Wakati wa kuongeza upatikanaji wa huduma ya kisasa ya nishati inaonekana kama kipaumbele muhimu ya maendeleo ya kimataifa - wakati tunajaribu kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) katika hali ya mazingira inayobadilika – STEPS Centre inaamini kwamba mbinu pana zaidi na kabambe za nishati na maendeleo inahitajika.

“Ifikapo mwaka 2030 idadi ya watu bila huduma ya umeme itapungua nukta isiyo na umuhimu wowote”

Upatikanaji wa kutofautiana wa huduma ya kisasa ya nishati

Rekodi ya kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya kisasa ya nishati inatofautiana duniani kote, mielekeo ya hali ya sasa inaonyesha kwamba maskini wataendelea



Solar-powered lighting, Sri Lanka_ World Bank Photo Collection

kutegemea vyanzo vya nishati za kitamaduni - kama vile mbao na taka hata hadi miongo ijayo. Ifikapo mwaka 2030 idadi ya watu bila huduma ya umeme itapungua kwa sehemu tu - kutoka bilioni 1.4 hadi bilioni 1.2, kulingana na takwimu kutoka Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na Shirika la kimataifa katika mambo ya Nishati (IEA). Nambari za wale wanaotegemea nishati za kitamaduni huenda hata ikaongezeka kutoka bilioni 2.7 kwa sasa hadi bilioni 2.8. Utegemezi wa nishati kutoka ujazo [wa kitamaduni] inatambuliwa sana kuwa na athari hasi kwa afya, elimu na ubora wa maisha, hata kuongeza na kuzidisha umaskini.

Suala la sera la haraka

Suala la sera la haraka Masuala haya yamedumu kwa muda mrefu zaidi na kwa sasa yamesababisha majadiliano ya kimataifa yanayoendelea kuhusu utawala wa hali ya hewa katika ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Mabadiliko ya hali ya anga (UNFCCC) lakini inaweka mkazo zaidi kutokana na umuhimu wa mkutano wa MDG na kushughulikia mabadiliko ya hali ya anga.

Kwa sera ya kimataifa, uharaka huu ni dhahiri katika utukizi wa mwaka 2012 kama Umoja wa Mataifa ya Mwaka wa Nishati Endelevu kwa Wote na Mkutano wa Rio+20 - Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo. Hakika, ilikuwa ni wakati wa Mkutano wa kwanza duniani wa [kiDunia: Earth Summit] katika mwaka 1992 kwamba UNFCCC ilizaliwa rasmi.

Tangu wakati huo, sera ya vyombo viwili vikuu imejengwa ambayo ni pamoja na, miongoni mwa mambo mengine, kuongeza upatikanaji wa nishati wakati wa kushughulikia mabadiliko ya hali ya anga- Kifaa cha Mazingira ya Ulimwenguni (GEF) na Mfumo Safi wa Maendeleo (CDM). Vyombo vyote viwili vinajaribu kufanya kutumia masoko ili kueneza teknolojia ya kaboni iliyopunguzwa lakini CDM, hasa, imeelekeza mabilioni ya fedha za kidola ya kuweka teknolojia hizo katika nchi zinazoendelea.

Malengo ya maendeleo yaliyokosekana

Hata hivyo, usambazaji wa miradi ya CDM inaakisi kumbukumbu inaturudisha kwenye ishara za hapo awali, zinazo onyesha kwamba upatikanaji wa nishati haulingani sawa sawa mahali pote. Nchi maskini zaidi katika dunia zinaendelea kukosa uwekezaji huu wakati baadhi ya nchi zinazoendelea (mfano Uchina, Brazili na India) zinavutia zaidi ya fedha na teknolojia za kaboni. Hata pale ambapo CDM imekuwa na mafanikio katika kuhamasisha fedha ya mradi ni tata jinsi “maendeleo” kwa kweli imefanikishwa, ama katika suala ndogo la kiteknolojia au katika suala pana la kibinadamu. Mafanikio yake inaonekana kuwa yamewekewa mipaka kwa matumizi ya baadhi ya aina ya maunzi ya kaboni kidogo, ikifuatana na ongezeko kidogo katika vibarua vidogo vidogo vya nchini. Kwa sababu hii, CDM haitaweza kuchangia maendeleo katika nchi nyingi. Kuzidisha, CDM haina uwezo wa kufanikisha baadhi ya aina ya endelevu.

Dhana pana ya teknolojia

Tunaamini hali hii mbaya inatokana na dhana ya kudumu ya teknolojia kama yenye ina maunzi tu. Dhana hii nyembamba imeelekeza maoni ya kwamba maunzi inaweza kuhamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine ambapo inaweza kuwekwa kwa matumizi kupitia rasilimali kidogo sana katika mafunzo na msaada. Kutokana na mawazo haya, tatizo kubwa katika kueneza teknolojia ni gharama zao, na ufumbuzi kuu ni fedha zinazofaa katika mahitaji kudumisha njia hizi za kiteknolojia].

“Maarika yanaofaa, ujuzi na uwezo wote yanahitajika ili kupitisha, kukabiliana na kuendeleza teknolojia, na pia kuzitumia”

Hata hivyo, kama sisi tutatambua teknolojia ambayo ni pamoja na sifa laini, kama vile elimu, basi tunaweza kuanza kuona kwamba vyombo vya sera kama CDM ni duni. Maarifa yanayofaa, ujuzi na uwezo inahitajika ili

kupitisha, kukabiliana na kuendeleza teknolojia, pia kuzitumia. Zote hizi kuna uwezekano zitatawanywa katika uchumi wowote wa taifa na zaidi, kutoa ongeleko la dhana kwamba teknolojia inapatikana katika mifumo. Bila makini na jinsi teknolojia zinasheha katika mifumo ya sasa au jinsi mifumo ya sasa inaweza kuendelezwa ili kuchukua teknolojia, sisi tunapunguza fursa za kutumia kwa mafanikio maunzi na kupuuza fursa zao za maendeleo.

Lakini, zaidi ya haya, teknolojia iko ndani ya desturi ya watu, au kumudu uwezekano wa desturi mpya. Mara nyingi teknolojia na desturi hushirikiana, kusaidia kueleza, kuzalisha au hata kuunda mazoea ya kiutamaduni. Na, bila shaka, udhibiti wa teknolojia unaweza kusababisha nguvu ya kiuchumi na kisiasa, hasa ni dhahiri katika teknolojia kubwa ya miundombinu kama vile huduma za gridi ya msingi ya umeme.

Kuelewa teknolojia katika maana hii pana - iliojengwa na kuwekwa na maarifa, ujuzi na uwezo - inatuwezesha kuchunguza matatizo makubwa ya mazungumzo ya kijamii, mifumo ya mazingira na kiteknolojia, na kutambua kwamba hakuna mwelekeo mmoja wa maendeleo unaepukika. Badala yake, njia nyingi za kutosha za maendeleo daima huwezekana.

Njia za nishati za watu maskini

Ufahamu huu inaongeza uwezekano zaidi kwamba njia za maendeleo mazuri zaidi kwa wat maskini na wanyonge zinaweza kukuzwa kwa njia ambazo zimeamuliwa-binafsi na kuelekezwa-binafsi. Hii haizuii matumizi ya mipango ya sera za juu-chini, badala yake, mipango hiyo inaweza kuwa sehemu ya zaidi ya kuunda-sera ambayo inatambua njia za faida nyingi za maendeleo hutegemea maarifa nyingi, ujuzi na uwezo katika michakato ya kuendelea kubadilika.



charcoal vendor, Zambia_CIFOR